# K.P.S.E.A
# TATHMINI YA SHULE YA MSINGI
# KAZI YA AGOSTI, 2026
# GREDI YA 6 -

## KISWAHILI KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA
## Muda: 20 KILA MWANAFUNZI

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

Jina: ______________________________ Shule: ______________________________

Nambari ya Tathmini: ______________________________ Tarehe: ______________________________

Nambari ya Shule: ______________________________ Sahihi: ______________________________

**MAELEKEZO KWA WANAFUNZI**

1. Andika jina lako, jina la shule yako na nambari yako ya mthani katika nafasi ulizoachiwa.
2. Andika tarehe,nambari ya shule yako kisa weka sahihi yako.
3. Soma kila swali kwa makini
4. Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote kwenye kijitabu hiki zimepigwa chapa.
5. Soma kifungu ulichopewa

**JEDWALI LA ALAMA**

| SEHEMU | INSHA | LUGHA | KUSI/KUZU | ASILIMIA (%) | KUZ 1 | KUZ 2 | KUF 1 | KUF 2 | KUK 1 | KUK 2 | CHI 1 | CHI12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KIWANGO CHA ALAMA | ALAMA 20 | ALAMA 30 | ALAMA 30 | | 90-100 | 75-89 | 58-74 | 41-57 | 31-40 | 21-30 | 11-20 | 1-10 |
| POINTI | | | | | 8 POINTI | 7 POINTI | 6 POINTI | 5 POINTI | 4 POINTI | 3 POINTI | 2 POINTI | 1 POINTI |
| JUMLA YA ALAMA ZA MWANAFUNZI | | | | | | | | | | | | |

## SEHEMU YA KWANZA: KUSILIKIZA NA KUZUNGUMZA (Alama 10)

## ZOEZI 1: MAISHA NA MASWALI YA PAPO KWA PAPO / ORAL QUESTIONS (ALAMA 10)

*Maagizo kwa mwalimu/mtahini: Msomee mwanafunzi maswali yafuatayo mmoja baada ya mwingine kisha uweke alama kulingana na uwezo wake wa kujibu kwa ufasaha na lugha sanifu. Kila swali lina alama 2.*

1. **Mwalimu:** Hujambo mwanafunzi? Naomba ujitambulishe kwa jina lako kamili, umri wako na gredi unayosoma.
   - **Mwanafunzi:** (Anatarajiwa kujibu: *Sijambo mwalimu. Jina langu ni... Nina umri wa miaka... na ninasoma katika Gredi ya Sita.*)
2. **Mwalimu:** Taja faida mbili tunazopata tunapotunza mazingira ya shule yetu kuwa safi.
   - **Mwanafunzi:** (Anatarajiwa kutaja faida kama vile: *Kuzuia magonjwa, kupendezesha shule, kupata hewa safi, au kuwa na mahali pazuri pa kusomea.*)

3. **Mwalimu:** Ukimkuta mwanafunzi mwenzako anaharibu vifaa vya shule kama vile madawati au vitabu, utachukua hatua gani?
    - **Mwanafunzi:** (Anatarajiwa kujibu: *Nitamwonya aache kufanya hivyo au nitaenda kupiga ripoti kwa mwalimu wa darasa/mwalimu mkuu.*)
4. **Mwalimu:** Ni somo gani unalolipenda zaidi hapa shuleni na kwa nini unalipenda somo hilo?
    - **Mwanafunzi:** (Anatarajiwa kutaja somo, mfano Kiswahili, Hisabati au Sayansi, na kutoa sababu inayoeleweka.)
5. **Mwalimu:** Ni nini maana ya methali hii: "Mtegemea cha ndugu hufa masikini"?
    - **Mwanafunzi:** (Anatarajiwa kueleza kuwa: *Methali hii inatufunza kuwa ni makosa kutegemea mali au msaada wa watu wengine badala ya kufanya kazi kwa bidii sisi wenyewe.*)

## ZOEZI 2: KUSOMA KWA SAUTI / ALOUD READING (ALAMA 20)

*Maagizo kwa mwanafunzi: Soma kifungu kifuatacho kwa sauti, ufasaha, na kwa kuzingatia alama zote za uandishi.*

Teknolojia ya kisasa imekuwa nguzo muhimu sana katika mfumo wa elimu nchini mwetu. Siku hizi, wanafunzi wengi katika shule za msingi wameanza kutumia vifaa vya kidijitali kama vile tarakilishi, vishkwambi na vibao-mbonyeo ili kurahisisha ujifunzaji wao. Matumizi haya ya vifaa vya kiteknolojia yanawasaidia watoto kupata maarifa mapya kwa haraka na kwa njia inayovutia sana.

Kupitia mtandao wa intaneti, mwanafunzi ana uwezo wa kusoma vitabu mbalimbali vya hadithi, kutafuta maana ya maneno magumu ya Kiswahili, na hata kutazama video za kimasomo zinazofafanua mada ngumu. Walimu nao wanatumia mbinu hizi mpya kuandaa masomo yao na kuwasilisha habari kwa njia ya picha na michoro inayoeleweka kwa urahisi darasani.

Hata hivyo, matumizi ya teknolojia yanahitaji uangalifu mkubwa sana kutoka kwa wazazi na walimu. Wanafunzi wanapaswa kuonyeshwa umuhimu wa kutumia mitandao kwa ajili ya masomo pekee, badala ya kupoteza muda mwingi wakicheza michezo ya video au kutazama mambo yasiyofaa. Matumizi mabaya ya vifaa hivi yanaweza kuathiri afya ya macho ya mtoto na hata kurudisha nyuma maendeleo yake ya kimasomo.

Tukitumia teknolojia kwa njia inayofaa na kwa kufuata maelekezo ya watu wazima, hakika itakuwa chombo cha thamani kubwa katika kutayarisha mustakabali mwema wa kizazi cha sasa na cha baadaye.

## MWONGOZO WA KUSAHIHISHA ZOEZI 2

*Mwalimu atathmini usomaji wa mwanafunzi kulingana na vigezo vifuatavyo (Jumla ya Alama 20):*

- **Ufasaha na Utamkaji wa Sauti (Alama 5):** Mwanafunzi anatamka maneno na sauti za Kiswahili kwa usahihi (bila kuchanganya sauti kama vile 'l' na 'r').
- **Kasi na Mtiririko (Alama 5):** Anashika kasi inayofaa; hasomi polepole sana kama anayeharajia au kwa kasi kubwa inayomeza maneno.
- **Kuzingatia Alama za Uandishi (Alama 5):** Anasimama kidogo kwenye mkato (koma) na kutulia kwenye kikomo (nukta), na kubadilisha sauti kwenye alama za nukuu au mshangao.
- **Sauti na Kujiamini (Alama 5):** Sauti yake inasikika vizuri darasani na anaonyesha utulivu na kujiamini anaposoma.